BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Sita – Tarehe 05 Disemba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub:

Hoja ya Mjumbe kuhusu kuliomba Baraza la Wawakilishi kutoa maazimio ya kushughulikiwa kwa haraka tatizo la kuharibika kwa vifaa tiba vya Hospitali ya Abdulla Mzee ya Mkoani Pemba.

Mheshimiwa Nassor Salim Ali:

Hoja ya Mjumbe kutaka Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuunga mkono hatua ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuingia Mkataba wa Mgawanyo wa Uzalishaji wa Mafuta na Gesi Asilia *(Production sharing agreement* – PSA).

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

109. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Mnada wa ng'ombe uliokuwa Chake Chake Mjini, ambao kutokana na kukuwa kwa mji, mnada huo sasa upo Meli tano. Lakini kwa mtazamo ng'ombe hutokea Kengeja, Kiwani, Chambani na maeneo mengine hadi kufika kwenye mnada huwa ni mbali sana.

(a) Je, Serikali wanalijua hilo.

(b) Je, hatua gani zimechukuliwa kama suala hilo linajulikana.

(c) Je, hatuoni kuwa ipo haja ya kuongeza mnada eneo la Chanjaani mpaka Chanjamjawiri ili kupunguza umbali.

Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

84. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale

Kutokana na agizo lililotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein la kufanyika kwa maonesho ya utalii kila mwaka nchini kwa lengo la kuendeleza utalii.

Je, Wizara imejipanga vipi juu ya agizo hilo.

<u>Wizara ya Fedha na Mipango</u>:

14. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Tume ya Fedha ya pamoja ilianzishwa kwa madhumuni ya kufuatilia vianzio vya mapato vya Muungano, lakini tangu kuundwa kwake hakuna faida iliyopatikana na Zanzibar kuendelea kutumia mgao wa asilimia 4.5% ambao umepitwa na wakati kutokana na kushuka kwa thamani ya shilingi na huku idadi ya Wazanzibari inaongezeka kwa kila mwaka.

(a) Je, Serikali inaweza kuwaambia wananchi Ripoti hii imekwama wapi ili waweze kufahamu.

(b) Je, lini Ripoti hii italetwa Barazani ili Wajumbe wapate kufahamu kazi ya Tume ya pamoja kuhusu gawio la Zanzibar katika vyanzo vya mapato ya Muungano.

90. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango iliahidi kutoa mafunzo ya ununuzi na uondoshaji wa mali za Umma kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Taasisi za Serikali kwa upande wa Pemba, pamoja na ununuzi wa gari ya Mamlaka kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2018/2019.

(a) Je, ni lini mafunzo haya watapatiwa walengwa hao.

(b) Je, gari hiyo kwa ajili ya Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji limeshanunuliwa.

<u>Wizara ya Afya</u>:

9. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya.

Kumekuwa na uzorotaji wa huduma katika wodi ya watoto ya Hospitali ya Mnazi mmoja ambapo wakati wa zamu za jioni na usiku anakuwepo Daktari mmoja na muhudumu mmoja tu katika ghorofa mbili zenye vitanda 36. Aidha, hali ya usafi katika jengo jipya lililojengwa kwa gharama kubwa hairidhishi.

(a) Je, Wizara itachukuwa hatua gani kuongeza Daktari na wahudumu katika wodi ya watoto kwa vile hao wawili hawatoshi kuhudumia wodi yote ukizingatia wao ni binaadamu na hivyo wanaweza kupata dharura.

(b) Je, hatua gani zitakazochukuliwa kuimarisha hali ya usafi wa jengo hilo.

10. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya.

Mnamo tarehe 18/07/2018 limetolewa dokezo na uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja lililonakiliwa Mheshimiwa Waziri wa Afya likielekeza wakuu wa Idara na Vitengo kuhakikisha wanachangisha baadhi ya huduma za wagonjwa wa sukari ambazo hazipatikani kama vile ‘stick sugar’.

(a) Je, kwanini huduma hizo zinakosekana.

(b) Kwanini wananchi wanachangishwa wakati Serikali imebeba jukumu la kutibu wananchi bure.

(c) Je, Waziri anatambua kuwa mzigo unaobeba Serikali ni mkubwa na anashauri nini ili kuisadia Serikali.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

40. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Katika sherehe ya ufunguzi wa siku ya chakula duniani iliyofanyika kwenye maeneo ya maonesho Chamanangwe Wilaya ya Wete tarehe 18/10/2018, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, alisema na kuwataka wakulima wetu wa Zanzibar kujikita zaidi katika kilimo cha muhogo kwani kuna mahitaji makubwa ya muhogo nchini China kutokana na matumizi mbali mbali ya muhogo na kuwataka wakulima wetu waache kulima muhogo kwa ajili ya chakula pekee na badala yake wajielekeze katika kilimo hicho kwa ajili ya biashara.

(a) Je, Wizara imeweka mkakati gani ili kuwaondolea wakulima wetu kulima kilimo hicho kwa ajili ya chakula na kuwawezesha kulima kwa ajili ya biashara.

(b) Je, Wizara itawasaidiaje wakulima hao kwa kuwapatia pembejeo na mbegu bora zenye uzalishaji wa kutosha wa muhogo ambao itakidhi viwango vya soko la Kimataifa.

(c) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Makampuni kutoka China ambayo yanataka kununua, yapo tayari kuwakopesha wakulima wa muhogo ambao wapo tayari kulima kwa wingi kwa ajili ya biashara.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

17. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto.

Hivi karibuni Mheshimiwa Waziri alishiriki katika hafla ya ugawaji wa vyarahani kwa akina Mama wa Jimbo la Kiembe Samaki na kuwataka wanawake wa majimbo mengine wajikusanye pamoja ili kupatiwa mikopo na Serikali.

Je, vikundi vya wanawake vilivyopo katika majimbo mengine vitapataje mikopo hiyo.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

44. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi kubwa za kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama. Hata hivyo kumekuwa na changamoto kubwa ya upungufu na wakati mwengine kukosekana kabisa kwa huduma hiyo katika baadhi ya maeneo. Kutokana na changamoto hiyo, baadhi ya wananchi huwa wanatumia mbinu mbadala za kutafuta huduma hiyo kwa kuchimba visima ndani ya maeneo yao.

(a) Je, ni utaratibu gani uliowekwa na Mamlaka ya Maji (ZAWA) unaotakiwa kufuatwa na wananchi wanaotaka kuchimba visima.

(b) Ni sababu zipi zinazopelekea mwananchi anaechimba kisima kwa kutumia gharama zake mwenyewe kutakiwa kulipia kisima hicho kwa Mamlaka ya Maji.

60. MHESHIMIWA MOH'D MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Katika kuhakikisha miji ya Zanzibar inapendeza na kuwa na hadhi ya kisasa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha mpango maalum wa uendelezaji wa miji yetu, ikiwemo ujenzi wa nyumba za kisasa katika miji iliyopangwa vizuri.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza miji iliyopo Pemba.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

78. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Je, ni hatua gani Wizara imefikia juu ya barabara ya Unguja Ukuu Kiembeni hadi Kisiwa cha Uzi ambayo imekuwa kero kwa wananchi kwa miaka mingi sasa.

79. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Katika kijiji cha Dunga, umaarufu Dunga mitini bado pamekuwa ni sehemu hatarishi kwa kukosa taa, alama za barabarani pamoja na matuta.

Je, kwanini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar isifanye maamuzi ya kuweka matuta ili kupunguza kasi za magari na ajali za mara kwa mara.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

51. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Katika miaka ya mwanzo ya 1980, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliwaruhusu wawekezaji mbali mbali kuanzisha viwanda ili kuwapatia wananchi wake ajira pia kuongeza pato la nchi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitoa maeneo makubwa ya ardhi kwa wawekezaji hao.

(a) Kwa kuwa viwanda vingi havifanyi kazi kwa muda mrefu mfano Cotex, Banco, Tan -Timber na kiwanda cha soda maruhubi Je, Serikali imechukua hatua gani kuirejesha ardhi hiyo Serikalini.

(b) Hivi ni sababu zipi zilizosababisha viwanda hivyo kufa kwa muda mrefu uliopita.

III. HOJA YA MJUMBE:

Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub:

Hoja ya Mjumbe kuhusu kuliomba Baraza la Wawakilishi kutoa maazimio ya kushughulikiwa kwa haraka tatizo la kuharibika kwa vifaa tiba vya Hospitali ya Abdulla Mzee ya Mkoani Pemba.

Mheshimiwa Nassor Salim Ali:

Hoja ya Mjumbe kutaka Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuunga mkono hatua ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuingia Mkataba wa Mgawanyo wa Uzalishaji wa Mafuta na Gesi Asilia *(Production sharing agreement* – PSA).

Zanzibar, **(Raya Issa Msellem)**
05 Disemba, 2018. **KATIBU WA BARAZA.**